



Salamu kutoka INDONESIA!

Jifunze kuhusu watoto
wa Baba wa Mbinguni
ulimwenguni kote.



KANISA LINALOKUA

Rais Russell M. Nelson aliwatembelea waumini
katika mji mkuu, Jakarta, mwaka 2019. Na
katika mkuano mkuu wa Aprili 2019, alitangaza
kwamba hekalu lingejengwa huko!



VOLKANO YA BLUU!

Indonesia inazo volkano hai
nyingi kuliko nchi nyininge
yoyote. Volkano ya Kawah Ijen ina
miale ya rangi ya bluu ambayo
inaweza kuonekana usiku.

VIELELEZO NA CONNER GILLETTE



Indonesia ni nchi iliyopo Kusini
Mashariki mwa bara la Asia. Ina
visiwa zaidi ya 17,000! Takribani
watu milioni 280 wanaishi huko.

MAHALI PA KUABUDU



Indonesia ina msikiti mkubwa
wa Kiislamu kuliko yote iliyoko Kusini
Mashariki mwa Asia. Ina hekelu
la Kibudha kubwa zaidi ulimwenguni.

JE, WEWE UNAZUNGUMZA LUGHA YANGU?



Kiindonesia ni lugha rasmi. Zaidi ya lugha
700 huzungumzwa huko Indonesia. Kauli
mbiu ya nchi yao inamaanisha "Wengi, lakini
mmoja" ili kuonesha kwamba ni wamoja.

NYUMBA YA MAJOKA

Majoka wa Komodo ndio mijusi
wakubwa zaidi ulimwenguni.
Wanaweza kukua hadi kuwa
urefu wa futi 10 (mita 3)!



KUCHORA BATIKI

Batiki ni aina ya sanaa ambayo
huongeza rangi kwenye nguo.
Unaweza kufanya kitu kama hicho pia!
Fanya usanifu katika karatasi
kwa kimiminika cha gundi. Gundi
inapokuwa imekauka, paka rangi
katikati ya mistari ya gundi kwa rangi
za maji.



NASI UDUK

- Osha **mchele mweupe vikombe 2.**
Loweka mchele katika maji kwa saa moja,
kisha chuja.
- Katika sufuria jingine, mimina **vikombe 2 vya tui la nazi.** Kisha ongeza **karaifuu 2 nzima, kijiti 1 cha mdalasini, na chumvi kijiko 1 cha chai.** Changanya na acha
mchanganyiko uchemke.
- Ongeza mchele kwenye mchanganyiko
huo. Funika na upike kwa moto wa chini
kwa dakika 15–20 hadi wali unapokuwa
umeiva.
- Uondoe kwenye moto na uache ukiwa
umefunikwa kwa dakika 10. Kula
na mayai ya kuchemsha, vitunguu
viliyokaangwa, au chochote kingine
unachopendelea.

**MAELEZO
YA UPISHI**

Hakikisha unapata
msaada wa mtu
mzima!



USINGIZI MZURI WA USIKU

Tunahitaji kulala ili tuwe na nguvu
ya kukimbia, kucheza na kufanya kazi.
Jaribu kulala muda uleule kila usiku.
Fanya kitu cha kukusaidia utilize akili
na mwili kabla ya kulala.

**KIDOEZO
CHA AFYA**

SHUGHULI